

REF: PPR/12- 1/11

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
TAREHE 05 DESEMBA 2011**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei elekezi na bei kikomo za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatatu, Tarehe 05 Desemba 2011**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo.

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa aina zote za mafuta zimebadilika kidogo ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 21 Novemba 2011. Katika toleo hili, bei za rejareja kwa Petroli zimeshuka, ambapo bei za Dizeli na Mafuta ya Taa zimepanda kidogo. Mabadiliko hayo ni kama ifuatavyo: Petroli imeshuka kwa TZS (30.54)/lita sawa na asilimia (1.51); Dizeli imepanda kwa TZS 40.74/lita, sawa na asilimia 2.00 na Mafuta ya taa imepanda kwa TZS 27.10/lita, sawa na asilimia 1.34. Mabadiliko haya ya bei za mafuta hapa nchini yametokana na mabadiliko ya bei katika soko la dunia na kuimarika kidogo kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani, (sarafu ambayo hutumika katika manunuzi ya bidhaa za mafuta kwenye soko la dunia). Bei za jumla kwa kulinganisha matoleo haya mawili zimebadilika kama ifuatavyo: Petroli imeshuka kwa TZS (30.54)/lita sawa na asilimia (1.56), Dizeli imepanda kwa TZS 40.74/lita, sawa na asilimia 2.07 na bei ya Mafuta ya Taa imepanda kwa TZS 27.10/lita, sawa na asilimia 1.39.
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na *fomula* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 5 la tarehe 9 Januari 2009 na marekebisho yaliyofanywa kupitia Tangazo la Serikali Na. 216 la Tarehe 29 Julai 2011.
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

	Bei Kikomo		
	Petroli (TZS/LT)	Dizeli (TZS/LT)	Mafuta Ya Taa (TZS/LT)
Dar es Salaam	1,990	2,075	2,049
Arusha	2,074	2,159	2,132
Arumeru (Usa West)	2,074	2,159	2,132
Karatu	2,092	2,177	2,151
Monduli	2,079	2,164	2,138
Ngorongoro (Loliondo)	2,130	2,216	2,189
Kibaha	1,994	2,080	2,053
Bagamoyo	2,001	2,086	2,060
Kisarawe	1,997	2,082	2,056
Mkuranga	1,999	2,085	2,058
Rufiji	2,017	2,103	2,076
Dodoma	2,048	2,134	2,107
Kondoa	2,081	2,166	2,140
Kongwa	2,046	2,131	2,104
Mpwapwa	2,050	2,135	2,108
Iringa	2,054	2,139	2,112
Kilolo	2,058	2,143	2,117
Ludewa	2,120	2,205	2,179
Makete	2,113	2,198	2,172
Mufindi (Mafinga)	2,063	2,149	2,122
Njombe	2,082	2,167	2,141
Bukoba	2,205	2,290	2,263
Biharamulo	2,179	2,264	2,238
Chato	2,162	2,247	2,221
Karagwe (Kayanga)	2,221	2,306	2,280
Muleba	2,205	2,290	2,263
Ngara	2,170	2,256	2,229
Misenyi	2,213	2,298	2,272
Kigoma	2,221	2,306	2,279
Kasulu	2,207	2,292	2,265
Kibondo	2,185	2,270	2,244
Moshi	2,063	2,149	2,122
Hai (Bomang'ombe)	2,067	2,152	2,125
Mwanga	2,056	2,142	2,115
Rombo (Mkuu)	2,084	2,170	2,143
Same	2,050	2,135	2,108

Siha (Sanya Juu)	2,070	2,155	2,129
Lindi	2,049	2,134	2,107
Kilwa Masoko	2,024	2,109	2,082
Liwale	2,069	2,155	2,128
Nachingwea	2,078	2,163	2,136
Ruangwa	2,076	2,161	2,134
Babati	2,112	2,197	2,171
Hanang (Katesh)	2,122	2,208	2,181
Kiteto (Kibaya)	2,123	2,208	2,182
Mbulu	2,125	2,210	2,183
Simanjiro (Orkasumet)	2,144	2,229	2,203
Musoma	2,168	2,253	2,227
Bunda	2,159	2,244	2,218
Serengeti (Mugumu)	2,213	2,299	2,272
Tarime	2,179	2,264	2,238
Mbeya	2,097	2,182	2,155
Chunya	2,106	2,191	2,165
Ileje	2,110	2,195	2,169
Kyela	2,112	2,198	2,171
Mbarali (Rujewa)	2,081	2,166	2,140
Mbozi (Vwawa)	2,106	2,191	2,165
Rungwe (Tukuyu)	2,106	2,191	2,164
Morogoro	2,015	2,100	2,073
Mikumi	2,030	2,116	2,089
Kilombero	2,052	2,138	2,111
Mahenge	2,063	2,148	2,122
Kilosa	2,033	2,118	2,092
Mvomero	2,025	2,111	2,084
Mtwara	2,062	2,147	2,121
Masasi	2,088	2,173	2,146
Newala	2,094	2,179	2,153
Tandahimba	2,087	2,172	2,146
Mwanza	2,140	2,225	2,198
Geita	2,180	2,266	2,239
Kwimba	2,176	2,261	2,234
Magu	2,148	2,233	2,206
Misungwi	2,145	2,230	2,204
Sengerema	2,172	2,257	2,231
Ukerewe	2,199	2,284	2,258
Sumbawanga	2,162	2,248	2,221
Mpanda	2,197	2,283	2,256
Nkasi	2,176	2,261	2,234
Songea	2,113	2,198	2,172

Mbinga	2,146	2,232	2,205
Namtumbo	2,142	2,228	2,201
Tunduru	2,172	2,257	2,230
Shinyanga	2,118	2,204	2,177
Kahama	2,132	2,217	2,191
Bukombe	2,144	2,230	2,203
Bariadi	2,160	2,245	2,218
Kishapu	2,146	2,232	2,205
Maswa	2,151	2,237	2,210
Meatu	2,158	2,244	2,217
Singida	2,080	2,166	2,139
Iramba	2,092	2,178	2,151
Manyoni	2,065	2,150	2,124
Tabora	2,144	2,229	2,202
Igunga	2,098	2,183	2,156
Nzega	2,108	2,194	2,167
Sikonge	2,155	2,241	2,214
Urambo	2,157	2,242	2,215
Tanga	2,036	2,121	2,095
Handeni	2,015	2,101	2,074
Kilindi	2,050	2,135	2,109
Korogwe	2,029	2,114	2,088
Lushoto	2,038	2,124	2,097
Mkinga (Maramba)	2,050	2,135	2,109
Muheza	2,036	2,121	2,095
Pangani	2,042	2,128	2,101

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Bei Kikomo-TZS/Lt	1,922.24	2,007.62	1,981.02

Haruna Masebu
MKURUGENZI MKUU
EWURA